



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO



**TAARIFA YA MAKAMU MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI e-GA KWA
NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA
UTAWALA BORA, MHE. RIDHIWANI KIKWETE (MB), WAKATI WA KUFUNGA
KIKAO KAZI CHA 4 CHA SERIKALI MTANDAO (e-GA)
FEBRUARI 08, 2024 KATIKA UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

***Mhe. Ridhiwani Kikwete (Mb); Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora,***

Mhe. Emmanuela Mtatifikolo Kaganda, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha,

***Ndg. Xavier Daudi; Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa
Umma na Utawala Bora,***

Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,

Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali,

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao,

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana;

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Awali ya yote, namshukuru mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kuhitimisha Kikao Kazi cha 4 cha Serikali Mtandao.

Mhe. Naibu Waziri, napenda kukushukuru kwa kukubali na kushiriki nasi katika kuhitimisha kikao kazi hiki. Tunafahamu unayo majukumu mengi ya kitaifa, lakini umetenga muda ili uweze kuwa nasi hapa leo.

Aidha, Bodi inatambua mchango wa wafadhili mliojitokeza katika kudhamini kikao kazi hiki, ahsanteni sana kwa michango ya hali na mali mliotoa. Tunaamini kuwa mtaendelea kutushika mkono katika vikao kazi vinavyofuata.

Nawashukuru viongozi wote wa Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na washiriki wote wa kikao hiki kwa kutenga muda wenu wa kuja kujumuika nasi hapa kwa muda wa siku tatu ili kwa pamoja tuweze kufanikisha juhudi za kujenga serikali ya kidijitali.

Kwa umuhimu wa kipekee nawashukuru Waandishi wa Habari kwa ushiriki wenu, kwani bodi inaamini kuwa, Waandishi wa habari ni wadau muhimu katika kuhamasisha matumizi ya Serikali Mtandao kupitia vyombo wanavyofanyia kazi.

Mhe. Naibu Waziri, Kikao Kazi hiki kimewakutanisha takribani wadau 1000 wa Serikali Mtandao na kujadiliana kuhusu mbinu za kuboresha utekelezaji wa jitihada za Serikali Mtandao. Kupitia majadiliano yaliyotokana na mada mbalimbali zilizowasilishwa wamefikia maazimio, ambayo Mamlaka itasimamia utekelezaji wake na kutoa mrejesho kwenye kikao kama hiki kijacho.

Leo hii, e-GA ipo tayari kupokea maelekezo yako kwa utekelezaji, sambamba na agizo la **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** la kuijenga Serikali ya Kidijitali, ambalo tunaamini litafikiwa kupitia jitihada za serikali mtandao zilizo imara na thabiti.

Mhe. Naibu Waziri, nihitimshe kwa kukushukuru tena kwa mara nyingine wewe pamoja na washiriki wote waliohuduria hapa leo.

Asanteni sana kwa kunisikiliza